**HALMASHAURI YA WILAYA YA MLIMBA**

**TAARIFA YA KIUCHUMI NA KIJAMII- (SOCIO-ECONOMIC PROFILE)**

## 1.0 UTANGULIZI

Halmashauri ya Wilaya ya Mlimba ni moja ya Mamlaka tisa (9) za Serikali za Mitaa zilizopo Mkoani Mororgoro. Halmashauri ipo umbali wa takriban kilomita 320 kutoka Makao Makuu ya Mkoa. Kwa upande wa mipaka, imepakana na Mji wa Ifakara na Manispaa ya Morogoro upande wa Kaskazini Mashariki, Wilaya ya Mufindi na Njombe upande wa Kusini na Kusini Magharibi inapakana na Wilaya ya Kilolo upande wa Kaskazini, na Wilaya ya Malinyi upande wa Kusini Mashariki.

**Eneo la Utawala:**

| **Halmashauri** | **Tarafa** | **Kata** | **Vijiji** | **Vitongoji** |
|---|---|---|---|---|
| **MLIMBA** | 2 | 16 | 62 | 244 |

Halmashauri ina eneo lenye ukubwa wa kilometa za mraba **6,924,** eneo hilo linajumuisha pia sehemu ya Pori la Akiba la Wanyama la Selous, Hifadhi ya Taifa ya Milima ya Udzungwa, na bonde la mto Kilombero ambalo hujaa maji  hasa kipindi cha masika.

## 1.2 Idadi ya watu

Kwa mujibu wa na taarifa za Sensa ya watu na makazi ya mwaka 2022, Halmashauri ya Wilaya Mlimba ina wakazi wapatao **292,536** kati yao wanaume ni **146,947** na wanawake ni **145,589** kutoka katika kaya **76,290** kwa wastani wa watu **3.9** kwenye kaya na ongezeko la wastani wa watu **3.2** kwa mwaka.

## 1.3 Hali ya Hewa na Uoto wa Asili

Hali ya hewa ya Halmashauri ya Wilaya Mlimba ni ya joto mithili ya pwani kwa wastani wa $26^o$ – $32^oC$. Kuna vipindi viwili vya mvua ambavyo ni mvua za vuli na mvua za masika. Mvua za vuli huanza kunyesha mwezi Novemba na kuisha mwezi Januari au Februari. Mvua za masika huanza mwezi Machi na kwisha mwezi Mei au Juni kila mwaka. Wastani wa mvua ni kati ya milimita 1200 hadi 1600. Sehemu kubwa ya Mlimba imo katika bonde la Mto Kilombero na kiasi kidogo kiko katika bonde la mto Rufiji na Pori la akiba la wanyama la Selous. Bonde la mto Kilombero linakingwa na milima ya Udzungwa ambayo pia ni Hifadhi ya Taifa ya Milima ya Udzungwa kwa upande wa Kaskazini. Milima hii imefunikwa na kupambwa na miti ya Miombo na baadhi ya wanyama ambao ni nadra kuwaona katika

Hifadhi zingine za Taifa na maeneo mengine duniani. Milima ya Udzungwa ina urefu wa meta 1,700 kutoka usawa wa bahari.

Kuna mito ipatayo 38 ambayo hutiririsha maji yake kwa mwaka mzima. Mito hiyo imekuwa na manufaa makubwa kwa Taifa katika utoaji wa umeme. Vyanzo vya umeme wa Kidatu na Kihansi vimo katika wilaya ya Kilombero. Pia imekuwa na manufaa kwa upande wa kilimo cha umwagiliaji hasa cha miwa, mpunga na ndizi.

## 1.4 Shughuli za kiuchumi

Zaidi ya asilimia 80 ya wananchi wa Mlimba hujishughulisha na kilimo. Wengi huzalisha, mpunga, mahindi, maharage na migomba. Mazao hayo hutumiwa kwa chakula na biashara. Hata hivyo, mazao makubwa ya biashara Mlimba ni mpunga, chikichiki, korosho, ndizi, ufuta na kakao. Mifugo pia ni sehemu ya uchumi wa Halmashauri. Mbali na kilimo shughuli zingine za kiuchumi ni uvuvi katika mto Kilombero na katika mabwawa na mito mingine iliyopo kwenye Halmashauri. Pia kuna makampuni ya uwindaji ambayo hufanya shughuli za uwindaji katika wilaya kando kando ya mto Kilombero na katika eneo la pori la akiba la Selous.

## 2.1 Mapato ya Halmashauri

Jukumu kubwa la Halmashauri ya Wilaya Mlimba ni kutoa huduma za kiuchumi na kijamii kwa watu wake. Katika kipindi cha miaka mitatu (3) kuanzia 2020/2021 hadi kufikia mwezi Juni, 2023 hali halisi ya makusanyo ya mapato ya Halmashauri ya Wilaya Mlimba ni kama ifuatavyo;-

**Jedwali Na. 1: Mapato ya Halmashauri Kutokana na Vyanzo Vyake;**

| **MWAKA** | **2020/2021** | **2021/2022** | **2022/2023** |
|---|---|---|---|
| **MAKISIO** | 2,700,000,000.00 | 3,080,000,000.00 | 3,025,000.00 |
| **MAPATO HALISI** | 2,590,012,062.60 | 3,469,255,832.13 | 4,077,349,293.61 |
| **ASILIMIA** | **96%** | **113%** | **135%** |

# 3.0 SEKTA YA ELIMU

## 3.1 ELIMU YA AWALI NA MSINGI

Halmashauri inazo shule **98** za serikali na shule **7** za binafsi zenye jumla ya wanafunzi **63,013**(Wavulana **31,484** na wasichana **31,529**).

3.2 **Uandikishaji kwa wanafunzi mwaka 2018-2020**

Takwimu zilizokusanywa hadi kufikia tarehe 31.03.2022 zinazoonesha wazazi wameitikia wito wa kuwapeleka na kuwaandikisha watoto wao shuleni, jambo lililopelekea kuvuka lengo la mwaka la uandikishaji. Hali hii imetokana na agizo la Serikali la kutoa Elimu Bila Malipo kwa shule za msingi na sekondari.

Uandikishaji wa wanafunzi shule za msingi katika Halmashauri ya Wilaya Mlimba umefanyika na kufungwa rasmi tarehe 31.03. 2022. Idadi ya wanafunzi walioandikishwa shuleni kwa kipindi cha miaka miwili hadi kufikia tarehe 31.03.2022 ni kama ifuatavyo:-

Mwaka 2023 Darasa la Awali walitazamiwa kuandikishwa wanafunzi wavulana 4,261, wasichana 3,369 jumla 7,630. Walioandikishwa wavulana 4,289, wasichana 4,090 Jumla 8,379 sawa na asilimia 109.8. Darasa la kwanza waliotazamiwa ilikuwa wavulana 3,852, wasichana 3,903 jumla 7,755. Walioandikishwa wavulana 4,313, wasichana 4,321 jumla 8,634 sawa na asilimia 111.3.

Mwaka 2022 Darasa la awali walitazamiwa kuandikishwa wavulana 3,417, wasichana 3,533 jumla 6,950. Walioandikishwa wavulana 4,059 wasichana 3,867 jumla 7,926 sawa na asilimia 114. Darasa la kwanza waliotazamiwa wavulana 3,701, wasichana 3,869 jumla 7,570. Walioandikishwa wavulana 3,965, wasichana 3,995 jumla 7,960 sawa na asilimia 105.

**Hali ya Miundombinu Shule za Msingi**

Halmahauri inaendelea kuhamasisha jamii kujitolea nguvu kazi kwa ajili ya ujenzi wa maboma kwa shule mpya ili watoto wasitembee mwendo mrefu kufuata huduma ya elimu. Hata hivyo shule shikizi zimeanzishwa kwa ajili ya kuwasaidia katika madarasa ya Awali, I - III.

**Hali ya Miundombinu na samani ni kama ifuatavyo: -**

- ✓ Madarasa mahitaji 1,401 yaliyopo 731 na upungufu 670 sawa na asilimia 52.2 ya madarasa yaliyopo.
- ✓ Nyumba za walimu mahitaji 1,401 zilizopo 208 na upungufu 1,193 sawa na asilimia 14.8 ya nyumba zilizopo.

- ✓ Matundu ya vyoo mahitaji wavulana 2,836 yaliyopo 979 na upungufu 1,857 sawa na asilimia **34.5** ya matundu ya vyoo yaliyopo.
- ✓ Madawati mahitaji **21,005** yaliyopo **14,795** na upungufu **6,210** sawa na asilimia 70.4 ya madawati yaliyopo.

**Takwimu za walimu**.

Hadi sasa Halmashauri inahitaji walimu 1,401 waliopo 795 na upungufu 606 sawa na asilimia **56.74** ya waliopo.

**Hali ya Ufaulu wa Wanafunzi darasa la Saba na la Nne 2020-2022**

Kiwango cha ufaulu kinaongezeka mwaka hadi mwaka kama ifuatavyo.

Mwaka 2020 Darasa la saba waliofanya mtihani wavulana **3,833**, wasichana **3,959** jumla **7,792**. Waliofaulu wavulana **3,644**, wasichana **3,737** jumla **7,381** sawa na asilimia 95 Darasa la Nne waliofanya wavulana 5,102, wasichana 5,200 jumla 10,302. Waliofaulu wavulana 5,059 wasichana 5,170 jumla 10,229 sawa na asilimia 99.29. Mwaka 2021 Darasa la saba waliofanya mtihani wavulana 2,938 wasichana 2,904 jumla 5,842. Waliofaulu wavulana 2,656 wasichana 2,617 jumla 5,273 sawa na asilimia 90.26 Darasa la Nne waliofanya wavulana 3,312 wasichana 3,473 jumla 6,785. Waliofaulu wavulana 3,092, wasichana 3,287 jumla 6,379 sawa na asilimia 99.

## 4.0 ELIMU YA SEKONDARI

Halmashauri ya Wilaya Mlimba ina Shule za Sekondari **31**. Kati ya shule hizo **25** ni za Serikali**, 5** ni za watu binafsi na **1** ni ya shirika la dini. Shule hizi zote ni za kidato cha kwanza hadi cha nne isipokuwa shule **3** (Nakaguru, Kiburubutu na Kilamsa sekondari) ambayo ni ya kidato cha kwanza hadi cha sita.

Idadi ya wanafunzi katika shule za Sekondari za Serikali ni **14,764** wakiwemo wavulana **7,005** na wasichana **7,759** Pia katika shule za binafsi kuna jumla ya wanafunzi **1,759** wakiwemo wavulana **670** na wasichana **1,089.**

## 4.1**.** Taarifa za Walimu

Halmashauri ya Wilaya Mlimba ina jumla ya walimu wa shule za sekondari za Serikali **416** kati yao **101** wanawake ni na wanaume ni **315**. Miongoni mwa walimu hawa **416**, walimu wa sayansi ni **132** na wa sanaa ni **284.**

## 4.3 HALI YA MIUNDOMBINU KWA SHULE ZOTE ZA SERIKALI

**Maabara**

Uhitaji ni jumla ya maabara **75** zilizopo ni maabara **42**.

**Vyumba vya madarasa.**

Uhitaji ni vyumba vya madarasa **459** kati ya **381** vinavyohitajika.

**Nyumba za Walimu**

Uhitaji wa nyumba za walimu **416** ili kuweza kukidhi haja ya upungufu wa nyumba za walimu katika shule zake. Kwa sasa kuna nyumba **56** tu hivyo kuna upungufu wa nyumba **360**.

**Matundu ya Vyoo**

Uhitaji wa matundu ya vyoo vya wanafunzi **475**; matundu yaliyopo ni **350** kwa wanafunzi wote, hivyo kuna upungufu wa matundu ya vyoo **125**. Hata hivyo, Halmashauri inafanya jitahada kila mwaka kwa kutumia mapato yake ya ndani na wahisani mbalimbali kuongeza matundu ya vyoo katika shule zake.

**Madawati**

Uhitaji wa samani kwa ajili ya wanafunzi ni meza **960** na viti **960**. Zilizopo ni **13,804** jitihada zinaendelea kufanyika hasa kutumia mapato ya ndani kupunguza tatizo la upungu samani hizo.

**Utoaji wa Chakula Shuleni**

Kutokana na agizo la Serikali kuwa shule zote za kutwa za Serikali zihakikishe kwamba zinatoa chakula cha mchana kwa wanafunzi, Halmashauri ya Wilaya Mlimba imafanikiwa kwa asilimia **100%** kutoa huduma hiyo katika shule zake zote za sekondari.

## 5.0 SEKTA YA AFYA

**Idadi ya Vituo**

Wananchi wa Halmashauri ya Wilaya Mlimba hupata huduma za afya kutoka katika vituo vipatavyo **48,** kati ya hivyo vya Serikali ni **27,** Mashirika ya Umma ni **4,** mashirika ya Dini ni **7** na watu binafsi ni **10.** Halmashauri inaendelea na ujenzi wa Hospitali ya Wilaya baada kupatiwa na Serikali Kuu **jumla ya Tshs.2,926,600,000.00** kwa kipindi cha **2020/2021** hadi mwaka 2022/2023 kati ya fedha hizo **Tshs. 376,600,000.00** zilikuwa ni kwa ajili ya ununuzi wa dawa na vifaa tiba. Serikali pia imeleta jumla ya **Tshs. 350,000,000.00** kwa ajili ya ukamilishaji wa Zahanati **7** ambapo Zahanati **6** zimekamilika na **1** ipo hatua ya kupakwa

rangi. Vituo vya Afya **4** vinaendelea kujengwa na vipo hatua ya ukamilishaji ambapo jumla ya **Tshs. 500,000,000.00** kutoka Serikali Kuu na **Tshs.1,380,000,000.00** kutoka kwenye mapato ya ndani ya Halmashauri zilitumika katika ujenzi wake.

**Huduma za Upasuaji wa Dharura Katika Vituo vya Afya**

Tangu mwaka 2021 vituo vya afya viwili (Mlimba na Mngeta) vimekuwa vikitoa huduma za upasuaji wa dharura kwa akina mama wajawazito.

**Usafi na Mazingira**

| **Kaya** | **Kaya zenye vyoo** | **Kaya zenye vyoo vya asili** | **Kaya zenye vyoo vilivyo boreshwa** | **Kaya zisizo na vyoo** |
|---|---|---|---|---|
| 46,353 | 46,353 | 5,052 | 41,301 | 0 |

## 6.0 SEKTA YA MAENDELEO YA JAMII

Sekta hii ni mtambuka. Ndani ya sekta yake kuna kitengo cha **UKIMWI**, uratibu, ufuatiliaji na usajili wa **NGOs;** ushirikishwaji jamii; maendeleo ya Jinsia na mtoto; na uwezeshaji kiuchumi na kupunguza umaskini, ambavyo kwa pamoja hufanya kazi ili kuboresha maisha ya wananchi wa Mlimba.

**Mapambano Dhidi ya UKIMWI**

**Kiwango cha Maambukizi ya Virusi vya UKIMWI 2020 - 2023**

| **Na.** | **Mwaka** | **KIWANGO CHA MAAMBUKIZI (%)** |
|---|---|---|
| 1 | 2020-2021 | 5.6% |
| 2 | 2021 - 2022 | 3.7% |
| 3 | 2022 - 2023 | 2.8% |

*Chanzo: Idara ya Afya*

## 9.0 UVUVI.

Shughuli za uvuvi ni shughuli kuu ya pili ya kiuchumi baada ya kilimo kwa wananchi wa Halmashauri ya Wilaya Mlimba. Shughuli hii inatoa ajira, inaongeza kipato na lishe bora kwa wananchi wa ndani na nje ya Halmashauri ya Wilaya Mlimba. Aina ya uvuvi unaotumika ni uvuvi wa nyavu, ndoano na uvuvi wa mitego ya asili. Kwa sasa shughuli za uvuvi zimeongezeka, hii imetikona na kundi kubwa la vijana na wanawake kujiajiri kupitia sekta ya uvuvi. Kitengo cha uvuvi kinatekeleza shughuli zake kwa mujibu wa Sheria,Sera

na Kanuni zake. Halmashauri ina zaidi ya watu 15,000 wanaojihusisha na shughuli za uvuvi na wote hawa wanategemea mito iliyopo kwenye bonde la mto Kilombero.

## 10.0 SEKTA YA MIFUGO

Shughuli za ufugaji katika Halmashauri ya Wilaya Mlimba ziliongezeka kwa haraka kuanzia mwanzoni mwa mwaka 1990. wafugaji wengi walihamia hapa na mifugo yao kutoka mikoa ya Arusha, Mwanza, Tabora, Shinyanga na Mbeya.

Eneo linalofaa kwa ajili ya mifugo ni hekta **54,000.** Kati ya eneo hilo, lililotengwa kwa ajili ya shughuli za malisho ya mifugo ni hekta **6,344.216**. Idadi ya mifugo baada ya zoezi la utambuzi,usajili na ufuatiliaji ni ng’ombe **103,783** mbuzi **28,287**, kondoo **26,456**, punda **126**, nguruwe **22,277**, kuku **272,272,** bata **33,368,** mbwa **13,999,** paka **4,797** na kanga **1,080**. Idadi ya wafugaji ni **5,683** na wote wamesajiliwa na kupewa vitambulisho maalum ya wafugaji.

## 11.0 SEKTA YA ARDHI

### Malengo yaliyowekwa

Halmashauri imejiwekea malengo ya kuhudumia wananchi kwa wakati ili kupunguza migogoro na kero zingine zinazo wakabili wadau wa sekta hii mtambuka. Halmashauri imeendelea na majukumu ya kuhudumia wananchi kwa kutoa elimu ya Sheria ya Ardhi Na. 4 ya mwaka 1999, Sheria ya Ardhi ya Vijiji Na. 5 ya mwaka 1999 pamoja na Sheria ya Mpango wa Matumizi ya Ardhi Na. 6 ya mwaka 2007 na Sheria ya Mipango Miji Na. 8 ya mwaka 2007.

### Taarifa ya upimaji wa mipaka ya vijiji Halmashauri ya Wilaya Mlimba

Halmashauri ya Wilaya Mlimba ina jumla ya Kata 16 na Vijiji 62 ambapo kati ya vijiji 62 vilivyopo, vijiji 61 vimepimwa mipaka yake ispokuwa Kijiji 1 cha Miyomboni. Kwakuwa vijiji vya Mpanga na viwanja 60 vina migogoro ya mipaka, Halmashauri inatarajia kuhakiki mipaka hiyo kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

### Taarifa ya hali ya mpango wa matumizi bora ya ardhi

Halmashauri ya Wilaya Mlimba ina jumla ya Kata 16 na vijiji 62 ambapo kati ya Kata 16, kata 6 ni maeneo ya mipango miji (planning area). Kata hizo ni Mchombe, Mngeta, Chita, Kalengakelu, Mlimba na Kamwene. Kati ya vijiji 62 vilivyoko katika Halmashauri ya Wilaya Mlimba, vijiji 61 vina matumizi bora ya ardhi isipokuwa Kijiji 1 cha Miyomboni kilichopo Kata ya Mofu hakina matumizi bora ya ardhi. Halmashauri kwa kushirikana na vijiji imefanikiwa kutenga maeneo ya hifadhi za misitu ya vijiji 7 yenye ukubwa wa hekta **13,785.92,** maeneo

ya malisho katika vijiji 19 yenye ukubwa wa hekta **5,047**, maeneo ya uwekezaji yenye ukubwa wa ekari **16,000** pamoja na maeneo ya viwanda vidogo katika vijiji **38**.

**Urasimishaji ardhi**

Halmashauri ya Wilaya ya Mlimba ina jumla ya vijiji 62. Kati ya vijiji hivyo, vijiji miji ni 4. Urasimishaji ardhi katika Halmashauri ya Wilaya Mlimba umekuwa ukifanyika kwa muda mrefu sasa chini ya uwezeshwaji wa MKURABITA, BRN na LTSP. Kupitia programu hizi tatu Halmashauri imeweza kupima mipaka ya vijiji, kuandaa vyeti vya ardhi vya vijiji, kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi, mipango ya kina katika vitovu vya vijiji pamoja na kuhakiki vipande vya ardhi na kutoa Hati za Haki Miliki ya Kimila.

## 12.0 Maliasili

Halmashauri ya Wilaya Mlimba ina aina mbalimbali za uoto wa asili kuanzia misitu minene hadi mbuga zinazofurika maji kwa msimu kila mwaka. Vile vile eneo la Mlimba lina mito **38** inayotiririsha maji mwaka mzima na kulifanya bonde la Kilombero kuwa chanzo cha **2/3** ya maji yote ya mto Rufiji. Hali hii imetoa fursa ya kuwepo kwa aina nyingi ya viumbe wakiwemo Wwanyamapori, mimea na samaki wa aina mbalimbali.

**Misitu ya Hifadhi**

Halmashauri ya Wilaya Mlimba ina maeneo ya misitu ya Hifadhi ya Serikali Kuu, Halmashauri na vijiji na Hifadhi ya Taifa ya Milima ya Udzungwa. Kutokana na kuhifadhi mazingira hasa misitu, mito mingi iliyopo kwenye Halmashauri imekuwa ikitiririsha maji mwaka mzima na hivyo kutumika katika shughuli mbalimbali kama vile kuzalisha umeme katika mgodi wa Kihansi na katika shughuli za umwagiliaji mashamba katika mashamba makubwa ya kuzalisha mpunga ya Kilombero Plantations Ltd (KPL) na katika mashamba ya wakulima wadogo wadogo.

**Upandaji miti.**

Shughuli hii inafanywa na wananchi kwa kushirikiana na wadau mbalimbali yakiwemo makampuni ya upandaji miti. Idadi ya miti iliyopandwa kwa mwaka 2022/2023 ni **2,053,007**.

**Wanyamapori**

Halmashauri ya Wilaya Mlimba imebarikiwa kuwa na Wanyama wa aina mbalimbali ambao wanapatikana katika Pori la Akiba la Kilombero na Hifadhi ya Taifa ya Milima ya Udzungwa. Aidha shughuli za uwindaji wa kitalii hufanyika katika pori hilo  la akiba, ambako kuna kitalu cha uwindaji cha Kilombero ruhudji/ ifinga GR West. Eneo hili lina wanyamapori aina ya Nyati, Simba, Chui, Fisi, Palahala, Pofu, Kongoni, Mamba, viboko, Kuro, na wengine wengi.

Vile vile wapo wanyamapori ambao hupatikana katika eneo la bonde la Kilombero pekee. Wanyama hao ni aina ya **Sheshe** ambao idadi toshelevu kwa maendeleo ya uwepo wa aina hii wanapatikana katika bonde hili. Hali kadhalika bonde la Kilombero lina jamii ya vyura adimu wanao nyonyesha maarufu kama vyura wa Kihansi (*Nectophryno idesasperginis)*.

## 12. SEKTA YA KILIMO

### Utekelezaji wa Malengo ya Kilimo.

Katika kutekeleza shughuli za sekta ya kilimo, Halmashauri ya Wilaya Mlimba, imezingatia miongozo na sera mbalimbali zinazotolewa kitaifa ambayo ni pamoja na:- **sera, sheria, mikakati na programu zinazosimamia masoko ya mazao ya kilimo kama vile:-**

- Sera: Kilimo ya Taifa (2013); Masoko ya Mazao na Bidhaa za Kilimo (2008); Maendeleo ya Ushirika (2002); Sera ya Taifa ya Umwagiliaji (2010) na Sera ya Taifa ya Biashara (2003).
- Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano (FYDP III) 2021/22-2025/26
- Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili (ASDP II) inayolenga kuwa na kilimo endelevu na chenye tija; kuongeza mapato ya wakulima; chanzo cha malighafi ya viwanda, kuongeza ajira, kuimarisha masoko na uratibu.
- Mazao ya asili ya biashara kama vile korosho na pamba yenye Bodi husimamiwa kwa mujibu wa Sheria ya uanzishwaji wa Bodi husika pamoja na marekebisho ya Sheria za Mazao ya Na. 20 ya mwaka 2009 [The crop laws (Miscellaneous amendments) Act 2009 ]
- Sheria ya Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Na.4 ya mwaka 2009, Sheria ya Afya ya Mimea Na. 4 ya mwaka 2020, Sheria ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko ya mwaka 2009 iliyorekebisha Sheria ya Usalama wa Chakula 1991 na agenda 10/30 Kilimo ni Biashara.Yote haya ni katika kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020-25.

### Hali ya chakula Halmashauri ya Wilaya Mlimba 2023/2024

Kwa mujibu wa taarifa za Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka **2022,** Halmashauri ya Wilaya Mlimba ina wakazi wapatao **292,536** kati yao wanaume ni **146,947** na wanawake ni **145,589** kutoka katika kaya **76,290** ambazo zinahitaji jumla ya tani **117,160.7** kwa ajili ya mahitaji ya chakula na ulinzi wa mkulima.

Mahitaji halisi ya chakula ni tani **109,701 (**wanga ni tani **98,730.9** na utomwili **(**protini) ni tani **10,970.1)** na ile ya ulinzi wa mkulima ni tani **7459.7**

Uzalishaji wa mazao ya chakula **2022/2023** ni tani **513,649.8** hivyo ikiwa ni ziada ya tani **396,489.13.**

Kwa Msimu **2022/23** lengo ilikuwa kulima Hekta **159,850** na kutarajia kuvuna tani **534,322.9**(kwa mazao ya chakula Hekta **148,278.5** na kutarajia kuvuna tani **477,729.9** za mazao mchanganyiko ya chakula. Mazao ya biashara hekta **9355.5** kwa tani **32,133.8** mboga na matunda hekta **2216.1** kwa tani **24,459.2).**

Utekelezaji halisi ni jumla ya hekta **167,650** kwa mavuno ya tani **555,472**(kwa mazao ya chakula hekta **154,236.5** kwa tani **513,649.8**. mazao ya biashara hekta **11,268.6**, kwa tani **17,568.5**, mboga na matunda hekta **2,145** kwa tani **24,254**. Hivyo ikiwa ni ziada kwa malengo yote tuliyojiwekea kwa ujumla.

**SHUGHULI ZA UMWAGILIAJI**

Halmashauri ya Wilaya Mlimba ina jumla ya mito 27 inayotiririsha maji mwaka mzima, na eneo linalofaa kwa njia ya umwagiliaji ni hekta **63,520,** kwa mchanganuo ufuatao:-

- Hekta **54,379** zinamilikiwa na jamii
- Hekta **9,141** zinamilikiwa na Taasisi za Umma (Magereza ya Idete hekta **1,000**, SUMAJKT Mngeta Plantation hekta **4,800** na Chita JKT hekta **3,341**)
- Hadi sasa eneo lililoendelezwa ni hekta **3,375 (hekta 3,000** za Taasis**i** na **hekta 375** zinamilikiwa na jamii**)** kati ya hekta **63,520** sawa na asilimia **5.3.**

Asilimia kubwa ya matumizi ya maji ya mito ni kwajili ya shughuli za kilimo na uvuvi hasa katika ngazi ya jamii, ambapo mito hiyo bado inatumia mfumo wa asili wa umwagiliaji. Hivyo jitihada zilizopo katika Halmashauri ya Wilaya Mlimba kwa sasa ni kuendelea kutenga bajeti ya kujenga na kuboresha miundombinu ya umwagiliaji itakayowezesha mfumo wa umwagiliaji kuwa wa kisasa na endelevu katika kipindi cha mwaka mzima. Aidha kwa sasa umwagiliaji unafanyika kwenye miundombinu iliyoboreshwa yenye kiasi cha Hekta 375 katika skimu ya umwagiliaji Njage, uzalishaji kwa zao la mpunga umeongezeka kutoka tani 1.2 kwa hekta hadi kufikia tani 4.5 kwa hekta.

## 14.0 SHUGHULI ZA USHIRIKA

- Kuendelea kusimamia na kushauri taratibu za kisheria kuzingatiwa na Vyama vyote vya Ushirika (Sheria ya Ushirika Na. 6 ya mwaka 2013) kuhusiana na kuzingatia uandishi wa vitabu vya hesabu, kumbukumbu na nyaraka muhimu za vyama.
- Kufanya uhamasishaji na uanzishaji wa vyama vya msingi vya mazao na masoko mchanganyiko katika kata mbalimabli na tayari Chama cha Uvuvi wa Kisasa Chita kimekabidhiwa nyaraka na kumbukumbu nyinginezo kwa ajili ya kwenda kukisajili kwenye Ofisi ya Mrajis Msaidizi Mkoani.
- Kuendelea na zoezi la maandalizi ya mauzo ya korosho kwa mfumo wa stakabadhi ghalani kwa msimu wa 2023/2024 kwa kushirikiana na Halmashauri za Malinyi, Ulanga na Ifakara Mji ikiwa ni msimu wa tatu.
- Kusimamia na kusuluhisha migogoro pale inajitokeza kwa haraka.

## 14.1 VYAMA VYA USHIRIKA WA MAZAO (AMCOS) NA MIKOPO (SACCOS)

Halmashauri ya Wilaya Mlimba ina idadi ya Vyama vya Ushirika vya Mazao vya Msingi (AMCOS) **5,** vyenye jumla ya wanachama **301** wakiwemo wanawake **67** na wanaume **234** mpaka Juni, 2023. Aidha Vyama vya Ushirika vya Mazao ya Kimkakati (Kakao na Korosho) vimefanikiwa kuuza mazao yao ambapo wanachama wameingiza kiasi cha Tshs. **117,950, 035** kwa Kakao na Tshs **19,201,369.60** kwa korosho na Halmashauri imepata Ushuru wa kiasi cha Tshs **2,601,450 na Tshs 692,390.40** mtawalia. Pia Halmashauri kwa kushirikiana na wadau mbalimbali iinahamasisha wananchi juu ya uundaji wa vyama vya akiba na mikopo (SACCOS), hususan kwa wakulima wa mazao ya kimkakati.

### BIASHARA

Katika kipindi cha kuanzia Julai 2020 hadi Juni 30, 2023, jumla ya Leseni za Biashara **2,257** zimetolewa na Leseni za Vileo **119** zimetolewa. Leseni za Vileo zimeingiza kiasi cha Shilingi **18,864,000.00** na Leseni za Biashara zimeingiza shilingi **333,928,900.00** kwa kipindi cha Julai 2020 hadi Juni 2022.

## 15.1 VIWANDA

Halmashauri ya Wilaya Mlimba ina viwanda vikubwa viwili ambavyo ni kiwanda cha kusindika mchele (KPL) na Mgodi wa Umeme wa Kihansi. Aidha kuna kiwanda cha kati kimoja ambacho ni Kiwanda cha Maji Laverna kilichopo Mbingu. Aidha, kuna viwanda vidongo **153.**